

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA MAKAMU WA RAIS  
MUUNGANO NA MAZINGIRA



BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

## TAARIFA KWA UMMA

**MWALIKO WA WARSHA YA KUKUZA UELEWA WA SHERIA YA USIMAMIZI  
WA MAZINGIRA NA KANUNI ZAKE IKIWEMO KANUNI YA VIWANGO VYA  
UDHIBITI WA KELELE NA MITETEMO KWA WAMILIKI WA KUMBI ZA  
STAREHE, BENDI, BAA NA WADAU WA MUZIKI**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeandaa Warsha kwa wamiliki wa kumbi za starehe, bendi, baa na wadau wengine wa muziki Mkoani Dar es Salaam, **siku ya Alhamisi Tarehe 30 Septemba 2021 saa 3:00 asubuhi katika ukumbi wa Mtana Multipurpose, uliopo Millenium Towers 2- Kijitonyama, Dar es Salaam.**

Lengo la warsha hii ni kukuza uelewa juu ya matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Viwango vya Udhhibiti wa Kelele na Mitetemo) za mwaka 2015. Aidha, wadau watapata nafasi ya kuainisha na kujadiliana changamoto mbalimbali na kutoa maoni juu ya namna bora ya kuimarisha udhibiti na usimamizi wa viwango vya kelele na mitetemo ili kuondoa athari kwa jamii. Mgeni rasmi katika Warsha hii ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhe. Selemani Saidi Jafo.

Hivyo, tunawaalika wadau wote kushiriki warsha hii muhimu, kwa kujisajili kupitia mawasiliano yafuatayo: **dg@nemc.or.tz, 0783 133 330 au 0755 878 001.** Mwisho wa usajili ni tarehe 28 Septemba 2021.

Imetolewa na:  
**MKURUGENZI MKUU**  
**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**  
**25 Septemba, 2021**